Mitalaa ya Shahada ya Uzamili ya Kiswahili: Mtazamo wa Urie Bronfenbrenner

Sheila Pamela Wandera-Simwa
Laikipia University, Kenya

Abstract

Kiswahili is one of the languages taught in many universities in Kenya at the level of certificate, diploma, bachelor's, master's and doctoral programmes. Generally, the teaching of Kiswahili in Kenyan universities and in East African universities has been there for the past four decades. Surprisingly, to date, in some of our universities, the curriculum offered still has the old courses that were taught four decades ago, not considering that there have been many metamorphoses since then. The curriculum used has not taken cognisance of these changes. Regrettably, the outcome is that it has ended up producing scholars with limited approaches to issues. In essence, a good curriculum should have certain specifics to produce a relevant professional in that specific area. This paper therefore, sought to analyse curricular from four universities in Kenya which offer master's programme in Kiswahili, to bring out the weaknesses and strengths of curricular on offer. The data is analysed using the tenets of the Bio ecological theory of Urie Bronfenbrenner and Ceci (1994), which was improved by Urie BronfenBrenner and Morris in 2007. The results of this paper will be useful in initiating curricular reviews of the Master's programmes in our institutions of higher learning with a purpose of harmonising the courses offered so that they are in tandem with the practice all over the world. In turn, this should be able to produce relevant master's students with the requisite and relevant training and experience.

Keywords: Bioecological theory, Kiswahili curriculum, master's programme, standardization.

Ikisiri

Kiswahili ni mojawapo ya lugha zinazofundishwa katika idadi kubwa ya vyuo vikuu nchini Kenya katika viwango vya stashahada, shahada, uzamili na uzamifu. Ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya, na hata Afrika Mashariki kwa jumla, umekuwepo kwa takriban miongo minne sasa. La kushangaza ni kwamba, kufikia sasa, bado zinafunzwa kozi zilezile zilizofunzwa miongo minne iliyopita pasipo kutambua kuwa maisha yanabadilika na sharti mitalaa pia ibadilike ili ikidhi mahitaji ya kisasa (Scott, 2008). Matokeo ni kwamba wanazalishwa wataalamu walio na mtazamo finyu, na waliolemaa kiusomi hasa wanapopimwa katika mizani ya kisasa. Mtalaa mwafaka sharti ushughulikie maswala mahususi ili uweze kuibua mtaalamu anayestahiki. Madhumuni ya makala hii ni kuchunguza mitalaa minne ya vyuo vikuu vinne nchini vinavyoandaa wazamili katika Kiswahili, na kujaribu kuangalia uzito na upungufu wayo katika kumwandaa mwanafunzi wa Kiswahili wa shahada ya uzamili. Data ilikusanywa kutoka Kalenda ya Mpango Mkakati za vyuo husika na pia katika idara mahususi vyuoni. Data hiyo imechanganuliwa kwa kuelekezwa na mihimili ya nadharia ya mtazamo wa mazingira ya mtu binafsi iliyoasisiwa na watalaamu Bronfenbrenner na Ceci (1994) na kuimarishwa na Bronfenbrenner na Morris (2007). Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Ni matarajio ya mwandishi kuwa mapendekezo ya makala hii yatasaidia katika kuchochea marekebisho na usawazisho wa kozi za Kiswahili za programu ya Uzamili ili ziweze kuafiki wakati, na hatimaye ziweze kuandaa wazamili mwafaka wa Kiswahili kupitia mtalaa mwafaka.

Maneno muhimu: Mtalaa wa Kiswahili, nadharia ya mazingira ya mtu binafsi, shahada za uzamili, usawazisho.

Utangulizi

Makala hii inahakiki mitalaa ya shahada ya uzamili ya Kiswahili kutoka vyuo vinne nchini Kenya ili kudadavua ni kwa kiasi gani mitalaa hiyo inamtayarisha mzamili wa Kiswahili na kukidhi mahitaji ya uzamili ipasavyo. Ili kufanikisha shughuli hii, makala hii imeanza kwa kuchunguza maana ya mtalaa. Hii ni kwa sababu kumekuwa na mitazamo mbalimbali kuhusu maana ya mtalaa kutegemea wanazuo mbalimbali. Baada ya kuangalia maana ya mtalaa, sifa za mtalaa mwafaka zimeweza kudondolewa kwa kurejelea wataalamu mbalimbali wa mitalaa. Sehemu hii ni muhimu kwa mwandishi kwa sababu baada ya majadiliano itawezesha kuarifu iwapo mitalaa ya Kiswahili ina sifa hii au la, na vipi inaweza kuboreshwa. Aidha, imeainisha mitalaa ya vyuo vinne teule nchini Kenya. Kozi katika mitalaa hii minne ndiyo data ya utafiti huu, na ndiyo itakayochanganuliwa ili kutupa mwelekeo kwa jinsi mitalaa ya programu ya Kiswahili nchini inavyoundwa. Sehemu ya nne ya makala hii imechanganua nadharia ya mazingira ya mtu binafsi ya Bronfenbrenner na wenzake kwa kuangalia mihimili yake. Nadharia hii ndiyo inayotumika katika kuchanganua mitalaa ya programu ya Kiswahili na basi ni muhimu kuielewa barabara kwanza. Sehemu ya tano inachanganua mitalaa hii kwa kuzingatia mihimili teule ya nadharia ya mazingira ya mtu binafsi. Kutokana na uchanganuzi wa mitalaa ya vyuo hivyo vinne kwa msingi wa nadharia, makala hii imeweza kutoa mapendekezo kwa waunda mitalaa ili waweze kuibuka na mitalaa mizuri inayokidhi mahitaji ya watumizi wake. Kauli za kuhitimisha ndizo zinazokamilisha makala hii.

Mfumo wa elimu ni taasisi ya kijamii ambayo inatarajiwa kubadilika kadri taasisi nyinginezo zinavyobadilika. Itakuwa jambo la kustajaabisha iwapo mfumo wa elimu wowote ule unatua palepale ilhali vitu vyote vile vinavyoizunguka, vinabadilika. Kuna haja ya kuhakikisha kuwa taasisi za elimu zinaendelea kukua, ili kujibu mahitaji ya mabadiliko katika jamii. Kukua kwa taasisi hizi pia kutaamsha ari ya kutaka kuulewa mfumo wa elimu barabara. Hali hii ya kutaka kuuelewa mfumo wa elimu ndiyo kiini cha masomo ya elimu na hususan masomo yanayohusiana na mitalaa (Seel na Dijikstra, 2004).

Mtalaa ni Nini?

Ross (2000) na Flinders na Thorntorn (2004) wanakubaliana kuwa neno mtalaa linatokana na neno la kigiriki linalomaanisha uwanja wa mashindano ya farasi, au mashindano yenyewe. Aidha, ni mahali ambapo mbio hizi za farasi zinafundishwa, ndiposa panapatikana dhana ya ufundishaji. Kwake Ross, kimsingi mtalaa ni matokeo ya ujifunzaji. Aghalabu mtalaa hurejelea ufafanuzi rasmi wa kile kinachofunzwa katika taasisi husika kulingana na matakwa yake. Pamoja na hayo, Ross (2000) anadokeza kuwa ndani ya mtalaa mahususi kuna mtalaa fiche: mtalaa ambao haujaainishwa, na ambao hupitishwa kwa kutokusudiwa kupitia mchakato mzima wa elimu. Kwa mweleko huu basi, mtalaa upo katika nyanja pana na unastahili kuhusisha shughuli za kijamii, ambazo zimeteuliwa kutoka utamaduni wa jamii husika na ambazo huchangia katika kumbadilisha mhusika. Seel na Dijkstra (2004) wanasema mtalaa ni maarifa na stadi katika maeneo mbalimbali ya somo ambayo walimu hufundisha wanafunzi ili wajifunze. Wanaendelea kusema kuwa mtalaa huwa na upeo na mipaka katika somo mahususi pamoja na mpangilio wa ujifunzaji. Kwamba, mtalaa huweka mbinu mahususi za kufikia malengo. Katika fafanuzi za wataalamu hawa dhana ya ujifunzaji kutokana na mtalaa imejitokeza bayana pasi na kusahau mchango wa utamaduni wa jamii husika katika kumuumba mhusika kupitia mtalaa mahususi.

Kulingana na Kridel na wengine (2010), kimsingi mtalaa unahusisha tajriba zinazopatikana na kupangika kwa namna ya kusababisha ujifunzaji, na hivyo elimu ya mitalaa kwao ni tathmini ya mchakato huu mzima. Nao Flinders na Thorntorn (2004) wanafafanua mtalaa kwa njia mbili. Kwanza, wanasema kuwa mtalaa ni tajriba zote zisizolenga pamoja na zile zinazolenga kuibua uwezo wa mhusika. Pili, wanasema kuwa

mtalaa ni msururu wa tajriba zinazolenga kufunzwa na ambazo hutumiwa na shule kukamilisha na kutimiza uibuaji wa uwezo wa mhusika. Kridel na wengine (2010) wanaelekeza kuwa mtalaa unahusisha uibuaji wa uwezo wa anayeutumia unaotokana na ujifunzaji kutokana na tajriba zote za kimaisha. Kwa mujibu wa makala hii tutapanua maana ya mtalaa kwa kusema kuwa mtalaa sio tu yale yaliyomo katika kozi ama eneo la somo kama walivyodokeza Seel na Dijkstra (2004), bali ni mapana na marefu ya programu nzima ya chuo-husika cha elimu. Mtalaa si kisawe cha silibasi kama wanavyochukulia watu wengi, kwa maana ya yaliyomo kwenye silibasi katika muktadha wa orodha ya masomo yatakayofundishwa, bali ni zadi ya hayo (Pinnar, 2003). Mtalaa ni mfumo mzima unaohusisha lengo, madhumuni, yaliyomo na matokeo yanayotarajiwa kutokana na mtalaa husika (Kelly, 2004). Hili linamaanisha kuwa vyuo vyahitaji kupanga mitalaa kwa ukamilifu wayo. Kwa hivyo, mtalaa unaotolewa na vyuo na kupokelewa na wanafunzi usiwe mkusanyiko wa masomo tofautitofauti, bali utazamwe kama programu moja kamilifu.

Kwa mwelekeo huu basi, mtalaa mwafaka lazima uwezeshe uchunguzi na tathmini ya kila mara. Lazima mtalaa huo uwezeshe shughuli zake za kielimu na kihuduma kukabiliana na mahitaji ya jamii ‘mpya’ inayobadilikabadilika (Scott, 2008). Kwa hivyo, mtalaa mwafaka ni ule unaoendelea kukua na kubadilika baada ya muda ili kukidhi mahitaji ya kijamii, na pia kuambatana na wakati (ISO, 2013; CUE, 2014). Aghalabu, mtalaa sio mwisho kiukamilifu, ila ni njia ya kufikia mwisho. Mtalaa hukuzwa ili utimize madhumuni ya elimu. Ni kifaa anachotumia mwalimu kuumba wanafunzi wake kulingana na madhumuni ya elimu katika mazingira ya mfumo rasmi. Mwalimu anakuwa msanii anayeumba sanaa yake kulingana na uhalisia wa mazingira yake. Mwalimu anachukua nafasi ya msanii, na mtalaa unachukua nafasi ya kifaa anachokitumia kuendeleza uwezo wa mwanafunzi wake kulingana na malengo ya elimu.

Sifa za Mtalaa Mwafaka

Scott (2008) anasema kuwa mtalaa mwafaka sharti uweze kuandamana na falsafa ya maisha. Ili hili litimilike, mtalaa huo huundwa kwa kuzingatia itikadi za kimaisha za taifa husika. Mila na desturi za taifa husika humulikwa katika nyanja zote, na pia vipengele vyote vya mtalaa mwafaka. Sifa hii maalum, huutambulisha mtalaa wa taifa husika miongoni mwa mitalaa ya mataifa mengine kwa sababu ya upekee wa taifa hilo. Kwa hivyo, mtalaa ulioundwa kwa kuzingatia itikadi za kimaisha za taifa husika utamzaa mwanafunzi aliye na imani katika itikadi hizo za taifa lake.

Ni muhimu pia kwa mtalaa kuweza kushughulikia ukuaji wa utu wa mhusika kwa sababu lengo kuu la elimu kwa jumla ni kumwezesha mhusika kuishi maisha ya ufanisi kutokana na ukuzaji wa uwezo wake. Mtalaa rasmi kwa hivyo hukuzwa kwa minajili ya kutekeleza lengo hilo la elimu. Shughuli za awali zilizopangiwa mtalaa huwa na majukumu ya kukuza utu wa mhusika. Katika muktadha huu basi, mtalaa sharti uwe na uwezo wa kukuza utu wa wahusika wake. Chuo kina jukumu la kumkuza mwanafunzi kupitia kwa mtalaa wake. Pamoja na hilo, mtalaa uweze kumwandaa mhusika kukabiliana na uhalisia wa maisha. Mtalaa mwafaka huhusisha kwa karibu matakwa ya maisha halisi. Wakuza mitalaa wahusishe mada zitakazowawezesha wanafunzi kuchangia katika shughuli za maisha ipasavyo, pamoja na kupata manufaa kwayo. Stadi zote, na shughuli zote zitakazohusishwa katika mtalaa ziwe zinazohusisha maisha halisi. Kwa kuwa jukumu la elimu ni kufundisha wanafunzi kwa minajili ya maisha ya baadaye, mtalaa umulike matakwa na mahitaji ya shughuli za kila siku za maisha. Taasisi za elimu zaweza kunasibishwa na jamii katika udogo wake, na hivyo zinapaswa kumwaandaa mwanajamii kukabiliana na matakwa ya maisha halisi. Shughuli za mitalaa huwafanya wanafunzi kufahamu mielekeo na matarajio ya jamii ili waweze kuwa wahusika bora katika maisha ya jamii. Hii tu ndio njia mwafaka ya kuamsha urazini wa kutatua matatizo ya kijumla. Chuo kina jukumu la kuwakuza kijamii wanafunzi

kwa kuwaandalia mtalaa uliotimilika, na utakaowawezesha kukabiliana na maisha halisi (Ross 2000). Kwa hivyo, kwa ukamilifu, mtalaa unastahili ushughulikie mahitaji ya mtu binafsi, na pia ya jamii kiutoshelevu. Nyanja zote zinazojenga utu wa mtu sharti zizingatiwe mtalaa unapoibuliwa. Lazima kuwe na nia ya kuwamotisha wanafunzi walio na uwezo mbalimbali. Mtalaa uzalishe wanafunzi watakaostawisha jamii toshelevu. Iwapo tofauti za kiutu miongoni mwa wanafunzi hazitashughulikiwa, basi hatutaweza kukuza utu miongoni mwao kiutoshelevu. Na ndio maana Kamisheni ya Vyuo Vikuu nchini Kenya (KAVVK) inapendekeza kuwa hatua ya kwanza na ya muhimu katika maandalizi na urekebishaji wa mtalaa wowote ule, ni kuwashirikisha wadau wote, mwanafunzi akiwa mdau muhimu, kwa kuwa ndiye mpokezi wa mtalaa huo (CUE, 2014). Hapa ndipo, mahitaji ya mtu binafsi, na yale ya kijamii hushughulikiwa kwa pamoja.

Mtalaa pia unastahili kuambatana na matakwa ya mtu binafsi. Mwanafunzi hastahili kupokezwa mtalaa, ila mtalaa unastahili kuundwa na kukuzwa ili kukidhi maslahi ya mwanafunzi, ikizingatiwa kuwa kila mja huzaliwa na uwezo fulani. Elimu hukuza na kupanga uwezo huo. Ili uwezo huo ukuzwe na kupangwa inavyostahiki, ni muhimu kwa mtalaa kuingiliana na miaka ya akili ya mtu, mahitaji yake ya kisaikolojia, mifumo yake ya ukuaji na pia kuzingatia tofauti za kibinafsi za watu. Mambo haya yakitiliwa maanani, madhumuni ya shughuli za mtalaa yataafikiwa inavyotarajiwa. Kwa mwelekeo huo, mtalaa mwafaka unafaa kuingiana na malengo ya elimu ya taifa husika. Aghalabu, mtalaa huundwa kwa kuzingatia madhumuni ya elimu. Njia muhimu na bora ya kufikia malengo ya elimu ni kuwa na mtalaa mwafaka. Mtalaa ambao hauhusishwi na malengo ya elimu, hauwezi kuzalisha wananchi wanaohitajika na taifa husika. Mtalaa ni mkakati na mpango marudufu ambao hulenga kuzalisha wananchi wanaotarajiwa na malengo ya elimu. Kwa hivyo, inaweza kusemwa kuwa mtalaa mwafaka ni kifaa cha kutambulisha malengo ya elimu ya taifa husika.

CUE (2014) inapendekeza kuwa mtalaa mwafaka ni ule unaoweza kunyumbulika ili kukabiliana na hali mbalimbali za mabadiliko ya kijamii. Mtalaa utaumbika kutegemea hali ilivyo. Kwa hivyo, mtalaa sharti uwe na chembechembe za kupindika, kuumbwa upya na hata kuimarishwa zaidi. Hii ni kwa sababu binadamu na jamii wanabadilika kila kuchao. Mabadiliko hayo yanaweza kuingizwa katika mada mbalimbali za mtalaa ili kizazi kipya kiweze kukabiliana ipasavyo na changamoto za dunia inayobadilika. Nchini Kenya, mitalaa ya vyuo vikuu hubadilishwa kila baada ya kila bembeo ili iweze kukabiliana na mahitaji ya wadau mbalimbali na pia mabadiliko ya kiwakati. Kwa kuwa mada na tajiriba za ujifunzaji zinazotokana na mtalaa mwafaka huwa zimechanganyikana na kuingiliana ni sharti basi mtalaa uwe na mshikamano na uendelevu. Chembechembe za mwendelezo na mpangilio mzuri hujitokeza bayana katika mtalaa mwafaka (Kelly, 2004). Mada na shughuli za mtalaa zinaposhikamana hukamilisha zoezi la ufundishaji na ujifunzaji ipasavyo kwa kulipa maana na kulifanya liwe na manufaa kwa wanaohusika. Shughuli katika mtalaa sharti zipangwe kwa namna ambayo zitawapa motisha wanafunzi kukabiliana na hali za baadaye. Hatimaye, ule mwendelezo wa tajiriba za ujifunzaji huchangia katika ukuzaji wa utu wa wanafunzi punde si punde.

Mtalaa mwafaka huuweka mfumo wa elimu, wanafunzi na walimu katika mwendo fulani wa mabadiliko, ambao kwa hakika huwa ndio msingi wa maendeleo (Seel na Dijkstra, 2004). Wakuza mitalaa wanaombwa kuhusisha katika mitalaa, shughuli ambazo zitasaidia ukamilifu wa ukuaji wa utu miongoni mwa wanafunzi ili waweze kuishi maisha yenye fanaka. Msisitizo katika mitalaa unastahili kutiwa katika shughuli za mazoezi ili wanafunzi wakuze vipawa vyao vya kubadilika na wakati. Mtalaa mzuri, kila mara, humshajiisha mwanafunzi kutenda, na pia huchangamsha akili yake, hivyo basi kumhuisha na kumwezesha kukubali mabadiliko. Katika muktadha huo, mada na shughuli za mtalaa zinastahili kuwa kamilifu, na zinazoweza kuleta mabadiliko ya kitabia miongoni mwa wanafunzi. Tajiriba za ujifunzaji zilizomo katika mitalaa zihusishwe na nyanja pana za maisha. Wanafunzi

wanapopitia tajiriba hizo, hupata ukamilifu katika kuelewa jamii na maisha. Mtalaa finyu hauwezi kukuza vipaji vya wanafunzi kikamilifu. Katika hali hii inakuwa muhimu kuumba tabia na mienendo ya wanafunzi kutegemea matarajio ya kitaifa, na itikadi zake kwa kutumia mtalaa ulio na shughuli zilizo kamilifu.

White (2005) anapendekeza kuwa mtalaa bora ni ule unaohusishwa na mahitaji ya mazingira yake. Mwanafunzi ni mwanajami na sharti awajibikie jamii yake. Kupitia elimu, mwanafunzi anawezeshwa kuelewa mazingira yake na mila za kimsingi, kusudi aishi maisha yenye fanaka. Pamoja na hayo, mtalaa mwafaka huchota kutoka kwa rasilimali na mafunzo ya kiteknolojia yanayopatikana katika mazingira husika ili kuimarisha ufundishaji. Hali hii humwezesha mwanafunzi kuelewa mambo yanayomzunguka barabara na ndivyo inavyopaswa kuwa katika mtalaa wa programu ya uzamili ya Kiswahili. Mtalaa mzuri basi hufundisha wanafunzi kuchukua nafasi yao katika jamii. Mtalaa mwafaka hukuza mtazamo bora wa jamii utakaokabiliana na changamoto na matatizo ya kijamii. Kupitia kwa mtalaa huo, mwanafunzi anaweza kuelewa majukumu yake ya kijamii kwa ukamilifu. Iwapo elimu ni mfumo wa kukuza maingiliano, basi mtalaa mwafaka utakuwa ule unaofanya kazi hii ya kutangamanisha wanajamii (Jardine, Friesen na Clifford, 2008). Mtalaa unastahili kumfanya mwanafunzi kufahamiana na desturi na amali za kijamii. Umfunze mwanafunzi sanaa ya kuishi kihalisia, na kuwafanya wawe raia wazuri. Katika hali hii, mtalaa utathibitisha kuwa mtekelezi mkuu wa mahitaji ya kijamii yanayofanya jamii kustawi, kuendelea na kukamilika.

Sifa nyingine ya mtalaa mwafaka ni uzingatiaji wa tofauti za kibinafsi miongoni mwa wanafunzi. Kila mwanafunzi huwa anazaliwa na uwezo wa kipekee unaomfanya awe tofauti na wenzake. Hizi tofauti za kipekee ndizo zinazoleta tofauti za kibinafsi. Wataalamu wanashikilia kuwa watu kwa jumla hutofautiana katika kile wanachopendelea, vijitabia na hata mielekeo (Slattery, 2008). Tofauti hizi kiuwezo miongoni mwa wanafunzi ni muhimu zikizingatiwa katika ukuzaji wa mtalaa. Ndio maana ni muhimu kuhusisha masomo ya lazima, yasiyo ya lazima, na hata ya ziada katika mtalaa ili wanafunzi waweze kuchagua masomo yao kulingana na mahitaji yao yanayotokana na upekee wao. Kama ilivyokwisha kutajwa hapo awali, katika mazingira ya Kenya, KAVVK inashurutisha kuhusishwa kwa wadau wakati wa kuibua na kurekebisha mitalaa. Ili kutekeleza hali hii, mtalaa lazima uhusiane na misingi ya kisaikolojia. Mahitaji ya kisaikolojia ya wanafunzi yazingatiwe wakati wa kukuza mtalaa mwafaka. Upendeleo na upeo wa mwanafunzi sharti uzingatiwe katika ukuzaji wa mtalaa. Ili malengo ya elimu yaafikiwe kwa ukamilifu, ni muhimu mada za mtalaa ziende sambamba na mahitaji ya kisaikolojia, mapendeleo na vijitabia vya kiasilia vya wanafunzi. Ndio sababu sharti mtalaa uzingatie uwezo mbalimbali wa wanafunzi. Mtalaa ukuzwe kwa sababu ya mwanafunzi na sio mwanafunzi kufuata amri za mtalaa. Ikiwa yanayofunzwa ni ya upeo wa juu kuliko uelewa wa wanafunzi, wanafunzi hawatapata motisha ya kutaka kujihusisha na ufundishaji. Katika hali hii, mfumo wote wa ufundishaji utakuwa haukusudii mwanafunzi, hauzalishi ari yake ya kutaka kujifunza na basi hauna maana. Kwa hivyo ni muhimu kuzingatia uwezo wa wanafunzi tunapoandaa mitalaa ya viwango mbalimbali vya wanafunzi.

Baada ya kupitia sifa za mtalaa mwafaka kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali, sehemu ifuatayo inatupa picha ya mitalaa ya programu ya uzamili ya Kiswahili katika vyuo vinne teule nchini Kenya ili baada ya uchanganuzi, iweze kubainishwa iwapo inasadifu sifa za mtalaa mwafaka kama zilivyodondolewa au la.

Mitalaa ya Programu ya Uzamili ya Vyuo Nchini Kenya

Makala hii inahakiki programu nne za shahada ya uzamili ya Kiswahili katika vyuo vikuu vinne nchini Kenya. Uteuzi huu wa vyuo hivi vikuu ulifanywa kimaksudi kwa kuzingatia ni lini shahada hii ilianza kufunzwa katika chuo husika, na iwapo vyuo ambavyo vilianza kufunza shahada ya uzamili hivi majuzi vimebadilisha chochote au la. Kwa hivyo kipengele

cha historia ya programu kiwakati kilizingatiwa sana. Chuo cha Nairobi ni cha kwanza kutoa mafunzo hayo, kikifuatwa na chuo cha Kenyatta. Chuo cha Egerton kilikuja baadaye, kisha cha Laikipia kikafuatia muda si mrefu. Mtafiti alipitia maelezo ya kila kozi iliyoorodheshwa hapa pamoja na mipangilio ya kozi zenyewe ili kuweza kupata picha kamilifu ya mitalaa ya programu za uzamili wa Kiswahili katika vyuo husika. Data hii, kama ilivyotajwa awali, ilipatikana katika Kalenda ya Mpango Mkakati za vyuo hivyo na idara mahususi. Lifuatalo ni jedwali la mitalaa ya program katika vyuo hivyo vinne:

Jedwali 1: Mitalaa ya Programu katika Vyuo vikuu nchini Kenya

Chuo Kikuu cha Nairobi	**Chuo Kikuu cha Kenyatta**	**Chuo Kikuu cha Egerton**	**Chuo Kikuu cha Laikipia**
Master's in Kiswahili	*Master's in Arts*	*M.A. (Kiswahili and Linguistics).*	*M.A. (Kiswahili and Communication).*
Research Methods	General Research Methodology	Mbinu za Utafiti katika Kiswahili	Mbinu za Utafiti katika Kiswahili
Advanced Swahili Phonology	Advanced Phonetics and Phonology	Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia	Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia
Advanced Mophology	Advanced Kiswahili Structure		
		Stadi za Mawasiliano	Kiswahili na Vyombo vya Habari
Literary Theories and Stylistics	Theories of Literary Criticism and Textual Analysis	Nadharia za Uhakiki	Nadharia za Uhakiki
Epic and Long Poems	Field Methods in Language Literature		
	History and Development in Kiswahili	Historia na Maendeleo ya Kiswahili	Historia na Maendeleo ya Kiswahili
Advanced Swahili Syntax	Trends in Linguistic Theory		
Semantics and Pragmatics		Sintaksia, Semantiki na Pragmatiki	Sintaksia, Semantiki na Pragmatiki
Advanced Swahili Prose	Contemporary Kiswahili Literature	Prose, Novel and Play	Fasihi Andishi na Mawasiliano
Advanced Swahili Drama	Children's Literature		
Swahili Poetry	Kiswahili Literature in History		
	Oral Literature in Kiswahili	Fasihi Simulizi	Fasihi Simulizi na Mawasiliano
Sociolinguistics		Isimu Jamii	Lugha, Jamii na Mawasiliano
	Discourse Analysis	Uchanganuzi wa Usemi	Uchanganuzi Usemi na Matini
Advanced Translation			Tafsiri na Mawasiliano
		Information Technology and Computer	

		Management	Lugha, Mawasiliano na Mahusiano Mema. Mbinu za Uhariri na Uchapishaji
Idadi ya kozi = 13	**Idadi ya kozi = 13**	**Idadi ya kozi = 11**	**Idadi ya kozi = 13**
Mradi	Mradi/ Tasnifu	Tasnifu	Tasnifu

Kimsingi, vyuo hivi vinne vinaandaa wanafunzi wa shahada ya uzamili ya Kiswahili ijapokuwa kila chuo kina jina mahsusi ya shahada inayotoa. Chuo kikuu cha Nairobi (CKN) ni '*Masters in Kiswahili'*, Chuo Kikuu cha Kenyatta (CKK) ni '*Masters in Arts (Kiswahili),* Chuo Kikuu cha Egerton ni *M.A. (Kiswahili and Linguistics)* na Chuo Kikuu cha Laikipia (CKL) ni *M.A. (Kiswahili and Communication).* Katika anwani za shahada kuna vyuo vinavyotumia Kiingereza kama vile CKN na CKK, ilhali vingine vinatumia Kiswahili na Kiingereza kama vile CKE na CKL. Vivyo hivyo, kozi na maelezo ya kozi katika mitalaa zimewasilishwa katika lugha ya Kiingereza kama vile katika CKN na CKK. CKE na CKL zimeorodheshwa kozi zao katika Kiswahili ila katika Kalenda zao za mpango mkakati, maelezo ya kozi katika CKE ni katika Kiingereza ilhali katika CKL ni katika Kiswahili. Pia, kuna programu ambazo zina kozi kumi na tatu kama vile CKN, CKK na CKL ilhali CKE ina kozi kumi za Kiswahili na moja ya Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Aidha, kuna kozi ambazo zinapatikana katika vyuo vingine lakini hazipo katika vyuo vingine kama vile kozi ya TEHAMA ipo tu katika CKE. CKK na CKE hazina kozi ya tafsiri. CKN haina kozi ya uchanganuzi usemi/matini. Pia, katika kutazama tu anwani za kozi, na hata baada ya kupitia maelezo ya kozi na mipangilio ya kozi hizo, ilikuwa wazi kwamba vyuo vingine bado vinafunza zile kozi za awali kabisa, kozi ambazo zilifunzwa miongo minne iliyopita, na ambazo hazitofautiani sana na kozi katika programu za shahada ya kwanza ila tu kwa matumizi ya neno 'advanced'. Kozi hizi ni kama vile: Advanced Swahili phonology, Advanced phonetics and phonology, Advanced mophorlogy, Swahili Poetry, Stadi za Mawasiliano, Children's literature na zinginezo.

Jambo lingine la kushangaza ambalo mtafiti alikumbana nalo alipozuru idara mahususi ni kwamba, hata katika wakati huu ambapo kuna wataalamu wengi mno ambao wana shahada za uzamifu katika Kiswahili, bado baadhi ya vyuo vinaandaa na kufunza baadhi ya kozi za Kiswahili kwa kutumia lugha ya Kiingereza kama vile CKE kozi ya Isimu Jamii, Uchanganuzi Matini na Mbinu za Utafiti zinafunzwa kwa Kiingereza. CKN na CKK hufunza kozi ya mbinu za utafiti katika Kiingereza. Pia, wanafunzi hao wa uzamili wanalazimishwa kuwasilisha pendekezo na matokeo yao ya utafiti kwa Kiingereza. Pamoja na hilo, kuna vyuo vingine pia ambavyo bado vinawakubali wanafunzi wa Kiswahili kuandika miradi na tasnifu za programu ya uzamili ya Kiswahili katika Kiingereza. Hili lilibainika katika CKK. Lililo bayana zaidi ni kwamba kila chuo kinaandaa programu yake pasipo kuzingatia mambo ya kimsingi kama wanavyoelezea Bronfenbrenner na Morris (2007) katika nadharia ya mazingira ya mtu binafsi. Wataalamu hawa wa mitalaa wanapendekeza kuwa programu zinapoandaliwa sharti zizingatie viwango vyote vya kozi zitakazofunzwa: kozi za kiada ambazo ni za lazima kwa mwanafunzi yeyote wa uzamili wa Kiswahili, kozi za umuhimu na kisha kozi za ziada kama inavyoonyeshwa katika mchoro 2. Kwa kifupi, mitalaa inapoandalia sharti mifumo inayotawala mazingira ya mtu izingatiwe ili mhusika aweze kufaidi kutokana na programu husika (Cunningham na Rosenbaum, 2015).

Baada ya kupata data ya utafiti huu kupitia picha ya mitalaa ya programu ya uzamili ya Kiswahili katika vyuo teule nchini Kenya, sehemu inayofuata inaelezea kuhusu msingi wa nadharia itakayotumika kuchanganua data hiyo.

Msingi wa Nadharia

Nadharia iliyotumika kuchanganua mitalaa ya programu ya uzamili nchini Kenya ni nadharia ya mazingira ya mtu binafsi. Nadharia hii iliasisiwa na Urie Bronfenbrenner katika mwaka wa 1979. Nadharia hii inazungumzia sifa za mtalaa mwafaka kwa njia ya kitaaluma. Mtaalamu huyu ameweza kufinyanga sifa hizo, kwa kuziweka kwa kile anachokiita mifumo ya kimazingira. Bronfenbrenner anatoa kauli kuwa, mtu ni zao la mazingira yake, ambayo humkuza na kumwendeleza, au kumdumaza. Mazingira haya yanaweza kuwa yale anayoingiliana nayo moja kwa moja, au yale asiyo na uhusiano wa karibu nayo, lakini yanayomwathiri kwa namna fulani. Mazingira anayoingiliana nayo moja kwa moja ameyaita mazingira ya karibu ilhali yale asiyoingiliana nayo kwa karibu mno ameyaita mazingira ya mbali.

Mara ya kwanza, Bronfenbrenner (1979) alipoibuka na nadharia hii ya mazingira ya mtu binafsi, aliweza kuainisha mifumo minne ambayo aliiweka katika ngazi nne ambazo hujenga ubinafsi wa mtu, mazingira yake na thamani yake katika jamii. Aliainisha mifumo hii kama mfumo mdogo (*microsystem)*, mwingiliano wa mifumo midogo (*mesosystem*), mfumo usio na uhusiano wa karibu na mhusika (*exosystem*), na mfumo mkubwa (*macrosystem*). Bronfenbrenner anaelezea mfumo mdogo kama mazingira yaliyo karibu sana na mhusika ambaye katika makala hii ni mzamili, na ambayo huweza kumwathiri kwa karibu sana. Anasema kuwa ni mambo ambayo mhusika huingiliana nayo kwa karibu sana. Masuala ambayo ni ya lazima na asiyoweza kuepukana nayo kwa namna yoyote ile. Katika kitengo cha pili, Bronfenbrenner anaelezea kuwa mazingira mbalimbali yaliyoko katika kitengo cha kwanza huweza kuingiliana na kumuathiri mhusika kama mshiriki mkuu. Kitengo cha tatu cha mfumo usio karibu na mhusika huhusisha mazingira ambayo hayamshirikishi mhusika moja kwa moja lakini anayoathirika nayo kwa jinsi ambavyo yanaingiliana na yale mazingira mengine ya awali. Kitengo hiki kinahusisha masuala yanayohusiana na mambo ya kijamii na kiuchumi (Boyd & Bee, 2006). Kitengo cha nne katika nadharia hii ni kile cha mfumo mkubwa. Hiki kitengo kinahusisha masuala ya itikadi, na amali za utamaduni ambazo mhusika amelelewa kwazo. Masuala haya huathiri mhusika kwani huwa amelelewa ndani yake, na yamekuwa kama sehemu yake.

Baada ya kung'amua kuwa ngazi hizo nne hazingeweza kukidhi mahitaji ya usasa yanayotokana na mabadiliko katika maisha, Bronfenbrenner aliweza kuimarisha nadharia yake kwa kuongezea ngazi nyingine ya tano aliyoiita mfumo mkubwa zaidi (*Chronsystem*). Mfumo huu unahusisha dhana ya wakati kama inavyohusiana na mazingira ya mtu binafisi. Vipengele vya wakati vinaweza kuwa vya ndani au nje ya mazingira ya mtu lakini vinamwathiri kwa namna fulani. Ufuatao ni mchoro wa jedwali la nadharia hii kulingana na Brofenbrenner (1994).



Mchoro 1: Ngazi za Nadharia ya Mazingira ya Mtu Binafsi ya Bronfenbrenner (1994)

Nadharia hii ya Bronfenbrenner imeweza kuhakikiwa na wataalamu mbalimbali wakiwemo Drakenberg (2004), Engler (2007), Drakenberg na Malgreen (2012), Drakenberg na Malgreen (2013) na Cunningham na Rosenbaum (2015). Wote wanatoa kauli kuwa ngazi tano za Bronfenbrenner hazitoshi kuhakiki masuala mahususi yanayopatikana katika jamii mbalimbali. Kila mmoja wao amejaribu kuongezea angalau ngazi zaidi ya zile za Bronfenbrenner, ili kukidhi mtazamo wake, na mahitaji yake ya kipekee.

Historia hii fupi ya nadharia ya Bronfenbrenner ya mazingira ya mtu binafsi ni muhimu kwa kuwa inaonyesha chanzo na maendeleo ya nadharia hii. Hata hivyo, kwa sasa kilicho muhimu ni jinsi nadharia hii inavyotumika kuchanganua mitalaa ya programu ya uzamili ya Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya. Sehemu hii imefafanua nadharia ya mazingira ya mtu binafsi na jinsi inavyoweza kutumika kuchanganua ufaafu wa mtalaa wa programu ya uzamili ya Kiswahili. Kwa kutumia maelezo ya nadharia hii, mwanafunzi yupo kati na anazungukwa na mtalaa kupitia kozi za programu. Kwa hivyo, mtalaa unawakilishwa na mazingira mbalimbali ya Bronfenbrenner. Je, mwanafunzi huyu anahitaji mazingira yapi kwa maana ya kozi zipi au mtalaa upi, ili akuzwe inavyostahiki? Je, mtalaa wa programu ya uzamili ya Kiswahili una sifa mwafaka za kumtosheleza kikamilifu huyu mwanafunzi aliye katikati ya mchakato mzima wa programu hii? Hayo ndiyo maswali yatakayojibiwa katika sehemu inayofuata, ya misingi ya nadharia katika muktadha wa mitalaa ya Kiswahili. Hivyo basi itakuwa bora kutazama mitalaa hiyo ya programu ya uzamili ya Kiswahili katika vyuo teule ili iweze kuchanganuliwa katika muktadha wa nadharia ya mtu na mazingira yake.

Misingi ya Nadharia katika Muktadha wa Mitalaa ya Kiswahili

Uchanganuzi wa mitalaa umeongozwa na mihimili ya nadharia ya mazingira ya mtu binafsi iliyoasisiwa na kuimarishwa na Urie Bronfenbrenner (1994, 1997, 2007). Nadharia hii inaainisha namna ambavyo mitalaa inastahili kuundwa ili ikidhi mahitaji ya programu husika. Katika makala hii ngazi tano za nadharia ya Bronfenbrenner (1994) zimefinyangwa katika ngazi tatu kuu kwa namna hii: ngazi za mfumo mdogo na mwingiliano wa mifumo midogo zinawakilishwa na kozi za lazima/kiada; ngazi za mfumo usio na uhusiano wa karibu lakini unaoathiri mhusika, na mfumo mkubwa zinawakilishwa na kozi za umuhimu; ilihali ngazi ya

mfumo mkubwa zaidi inawakilishwa na kozi za ziada. Mchoro 2 ufuatao unaelezea kwa kina zaidi:



Mchoro 2: Uchanganuzi wa kozi za programu ya uzamili ya Kiswahili

Matokeo ya Utafiti

Kozi za kiada/lazima

Kozi katika kitengo hiki zinawakilisha ngazi mbili; ya mfumo mdogo, na mwingiliano wa mifumo midogo. Kwa hivyo, hizi ni kozi ambazo mwanafunzi wa programu ya shahada ya uzamili sharti azipitie ili afuzu kuitwa mzamili wa Kiswahili kwa sababu ni za karibu sana kwake na zitamwathiri ipasavyo kama msomi wa Kiswahili. Kozi hizi ni kama vile:

- Mbinu za Utafiti katika Kiswahili
- Historia na Maendeleo ya Kiswahili
- Kozi ya tafsiri
- Fasihi ya Kiswahili
- Isimu ya Kiswahili

Kozi za Umuhimu

Kozi hizi pia zinawakilisha ngazi mbili; ya mfumo usio karibu na mhusika lakini unaomwathiri kwa namna fulani, na mfumo mkubwa ambao mara nyingi huhusisha itikadi na amali za utamaduni unaomlea mhusika. Japo zipo mbali na mhusika huathiri utaaluma wa mwanafunzi kwa namna fulani, na kwa hivyo ni muhimu sana kuwepo katika mtalaa mzima:

- Uchanganuzi usemi na matini
- Nadharia mbalimbali za Uhakiki
- Isimu Jamii
- Fasihi Simulizi na utafiti nyanjani
- Kozi za Mawasiliano

Kozi za Ziada

Kitengo hiki kinalandana na ngazi ya mifumo mikubwa zaidi ambayo ni mazingira ya juu kabisa kulingana na Bronfenbrenner (1994). Ngazi hii huhusisha mambo ya kihistoria

ambayo yamekuwa pale katika kipindi kirefu na ambayo yalishika mizizi, na hivyo kuwa na athari kubwa kwa mhusika. Mambo haya si ya lazima, lakini yanafaa kushughulikiwa kwa sababu yana mchango wake kwa mtu binafsi, na basi kwa wale ambao wameathirika pakubwa kwayo, wanaweza kushughulikiwa kupitia kozi kama zile, lakini ukweli ni kwamba hazina lazima yoyote. Kutokuwepo kwa kozi hizi hakuwezi kuathiri utaalamu wa mwanafunzi:

- Kiswahili na Vyombo vya Habari
- Lugha, Mawasiliano na Mahusiano Mema
- Mbinu za Uhariri na Uchapishaji

Kwa kutazama kozi zinazofundishwa katika vyuo hivi vinne vinavyotoa mafunzo ya shahada ya uzamili katika Kiswahili, inadhihirika pia kuwa kuna haja ya kuoanisha baadhi ya kozi katika vyuo husika, ili kuzua nafasi ya wanafunzi wa Kiswahili kutanda katika mawanda mapana hasa inapozingatiwa kuwa wanahitajika kutaalamika katika vitengo vitatu kwa pamoja: fasihi, lugha na isimu. Shughuli hii inaweza kusimamiwa na taasisi mbalimbali zinazohusiana na masomo ya vyuoni kama vile Kamisheni ya Masomo ya Vyuo Vikuu nchini Kenya (KAVVK), Kamisheni ya Masomo ya Vyuo Vikuu Afrika Mashariki (KAVVAMA) au Kamisheni ya Kiswahili Afrika Mashariki (KAKAMA). Usawazisho huu usipotiliwa maanani, kuna vyuo ambavyo vitawatoa wanafunzi ambao wameegemea upande mmoja tu, na kupuuza mwingine.

Mapendekezo

Baada ya uchanganuzi wa mitalaa ya programu ya shahada ya uzamili wa Kiswahili katika vyuo vinne vya kitaifa, makala hii inapendekeza yafuatayo:

i) Imebainika kuwa kozi zinazofunzwa zinatofautiana kutoka chuo kimoja hadi kingine. Ijapokuwa hali hii ni bora kwa kuwa inaleta ladha, na pia inachangia upekee wa chuo, ni muhimu kozi za kimsingi/ kiada (mfumo mdogo) zishabihiane kwa kiasi kikubwa kwa sababu ndizo zinazomtambulisha Mzamili wa Kiswahili

ii) Kutokana na udurusu wa mipangilio ya kozi zinazofunzwa katika baadhi ya vyuo teule, inabainika kuwa kozi hizo zimeandaliwa kwa namna ambavyo ufundishaji wake unamlenga mhadhiri pakubwa. Kuna umuhimu wa kuandaa kozi zile upya ili ziweze kumlenga mwanafunzi ambaye ni mzamili kwani ndiye anayepaswa kuathirika na masomo yale na wala siyo mhadhiri. Mtindo wa kumlenga mhadhiri ni wa kale na umepitwa na wakati.

iii) Pamoja na hili la kumlenga mhadhiri, maudhui katika baadhi za kozi za uzamili za Kiswahili kama zilivyopitiwa, yamepitwa na wakati katika kiwango hiki kwa kuwa yalishughulikiwa kwa undani katika shahada ya kwanza, na hamna la ziada linaloongozewa ila neno ‘advanced’ na mifano mingi mingi tu. Kwa mfano kozi kama vile ‘Advanced Phonetics and Phonology’, ‘Advanced Morphology’ ‘Advanced Kiswahili Structure’, ‘Advanced Swahili Prose’, ‘Advanced Swahili Drama’ na ‘Advanced Syntax’ . Maudhui yanafaa kuimarishwa ili yaandamane na wakati, kwani mambo mengi yamebadilika. Ni muhimu kuunda kozi mpya zilizo na soko au kukarabati zile zilizoko ili ziweze kumudu mahitaji ya kisasa. Njia rahisi ya kufanya hivyo ni kuzingatia sifa za mtalaa mpya kama zilivyoorodheshwa hapo awali.

iv) Lugha hubeba utamaduni wa jamii husika. Kupitia kwa lugha tumizi baadhi ya tamaduni za jamii husika huweza kuwasilishwa na kupitishwa kwa wahusika. Kwa mkondo huu, ni muhimu kwa wahadhiri kuzingatia matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kufunzia kozi za Kiswahili ili dhana ya utamaduni ijitokeze barabara katika mtalaa mzima, kwani kama anavyodokeza Ross (2000) mtalaa

mwafaka ni ule unaozingatia utamaduni wa jamii husika ili mwanafunzi aweze kukuzwa kiukamilifu huku akithamini mila na desturi za jamii inayomlea.

v) Mitalaa ya programu za uzamili inapoandaliwa au hata kurekebishwa baada ya muda uliowekwa na sheria (CUE, 2014), ni muhimu kuegemeza swala nzima katika nadharia za uundaji mitalaa, au vizuri zaidi kuwaalika wataalamu katika nyanja hiyo, ili shughuli hiyo ifanywe ipasavyo. Kutowashirikisha wataalamu wa mitalaa, wadau, pamoja na wajuzi wa nyanja husika ndiko kunakosababisha uundaji wa mitalaa finyu ambayo inaleta upungufu katika programu husika, na hatimaye kusababisha utoaji wa wazamili ambao wamepungukiwa kitaaluma.

Katika kuunda mtalaa wowote ule kama anavyopendekeza Kelly (2004) ni muhimu kuuliza maswali yafuatayo:

- Kwa nini mtalaa huu unaundwa? Hapa linaloshughulikiwa ni lengo au madhumuni ya mtalaa.
- Ni nini kilicho ndani ya mtalaa huu? Kwa kujibu swali hili linaloshughulikiwa ni maudhui au mada katika mtalaa mzima
- Mtalaa huu utafunzwa vipi? Swali hili litasaidia katika kutayarisha mbinu za ufundishaji kama vile vitabu vitakavyohitajika, vifaa vya kufunzia, jinsi ya kufundisha kama ni kupitia mijadala, mihadhara na mbinu zinginezo.
- Matokeo yake yatakuwa yapi? Katika kitengo hiki kinachoshughulikiwa ni matarajio ya mtalaa. Hili ni jambo muhimu kwa sababu linatoa maono kuhusu aina ya mzamili anayezalishwa kutokana na mtalaa husika.

Hitimisho

Kila nadharia ina upungufu na uzito wake, lakini kwa kiasi kikubwa nadharia hii ya mazingira ya mtu binafsi, inathibitisha kuwa Mzamili wa Kiswahili ni zao la mazingira yake ya karibu na ya mbali ambayo yanatokana na mtalaa anaoupitia. Baadhi ya mazingira, kwa maana ya mtalaa wa programu ya uzamili katika makala hii, yamechangia ufinyu wake kwa sababu ya jinsi yalivyokuzwa. Kuna wakuza mitalaa ambao hawazingatii kanuni za uundaji mitalaa thabiti, na mwishowe wanaibuka na kozi finyu ambazo haziwezi kumkuza mwanafunzi kitaaluma.

Makala hii imeweza kubainisha kuwa baadhi ya mazingira anayotagusana nayo mzamili wa Kiswahili yana chembechembe za mapengo kwa kiasi fulani, na ambayo yanahitaji kuzibwa ili kumjenga na kumkuza mzamili anayestahiki. Sifa za mtalaa mwafaka zilizopitiwa katika sehemu ya pili ni nzuri kwa sababu zinaweza kutumika kutathmini maudhui ya mitalaa katika viwango mbalimbali vya masomo ikiwamo kiwango cha shahada ya uzamili. Kwa kuelekezwa na sifa za mtalaa mwafaka, pamoja na nadharia ya Bronfenbrenner ya mazingira ya mtu binafsi, huku ikishadidiwa na mapendekezo ya KAVVK imebainika kuwa mitalaa ya programu ya uzamili ya Kiswahili ina upungufu na uzito pia. Bronfenbrenner amesaidia kubainisha kuwa mzamili wa Kiswahili ni zao la mtalaa anaokumbana nao katika safari yake ya usomi. Mtalaa ukiwa na upungufu unamzaa mzamili aliyepungukiwa, lakini ukiwa umekamilika bila shaka unamzaa mzamili aliyekamilika.

Marejeleo

Boyd, D., & Bee, H. (Eds.) (2006) *Lifespan development* (4th Edition). Boston: Pearson Education.

Bronfenbrenner, U. (1979) *The Ecology of Human Development*. Cambridge. M.A: Harvard University Press.

Bronfenbrenner, U., & Ceci, J. (1994) Nature-nurture reconceptualization in development perspective: a bioecological model. *Psychological Review, 101,* (4) 568-586.

Bronfenbrenner, U., & Morris, P. A. (2007) 'The bioecological model of Human Development'. In W. Damon & R. M. Lerner (Eds.) *Handbook of Child Psychology (*6th Edition) Vol.1 (pp. 793-823). New Jersey, Hoboken, NJ: Wiley.

Cunningham, B. J., & Rosenbaum, P. L. (2015) A bioecological framework to evaluate communicative participation outcomes for pre-schoolers receiving speech-language therapy interventions in Ontario, Canada. *International Journal of Language & Communication Disorders, Vol. 50,* No. 4, 405-415.

Commission for University Education [CUE] (2014) University guidelines and standards programmes. Retrieved November 2015, from http://www.cue.or.ke

Drakenberg, M., & Malgren, T. (2012) Basic values: Are curriculum ideas being realised? A metaphor analysis. *Citizenship, Social and Economic Education, 11* (2), 77-88.

Drakenberg, M., & Malgren, T. (2013) School principals' perceptions of 'basic values' in the Swedish compulsory school systems in regard to Bronfenbrenner's ecological systems theory. *Citizenship, Social and Economic Education, 12,* Number 2, 2013. Retrieved July 9, 2018, from www.wwwords.co.ke/CSEE

Engler, K. (2007) 'Bronfenbrenner revised in the 21st Century: A look at how the ecological systems theory may be inadequate.' A Capstone project submitted in partial fulfilment of the requirements for the Master of Science Degree in counsellor educational at Winom State University.

Flinders, D., & Thornton, J. S. (2004) *The curriculum studies reader*. Milton Park, Abingdon, Oxon, UK: Routledge Falmer.

International Standards Organisation [ISO] (2015) *Quality management principles.* Retrieved Retrieved March 2017, from www.iso.org

Jardine, D.W. Friesen, S., & Clifford, P. (2008) *Curriculum in abundance.* Mahwah (NJ): Lawrence Erlbaum Associates, Inc., Publishers.

Kelly, I. V. (2004) *Curriculum theory and practice*. Sage Publications Limited UK. London

Kridel, C. (Ed.) (2010) *Encyclopaedia of curriculum studies.* A Thousand Oaks (CA): Sage Publications.

Pinar, W. (2003) *International handbook of curriculum research*. Mahwah (NJ): Lawrence Erlbaum Associates, Inc. Publishers.

Ross, A. (2000) *Curriculum: construction and critique*. USA: Taylor & Francis.

Scott, D. (2008) *Critical essays on major curriculum theorists*. Milton Park, Abingdon, Oxon, UK: Routledge.

Seel, N. M., & Dijkstra, S. (2004) *Curriculum, plans, and processes in instructional design: International PERSPECTIVES.* Mahwah (NJ): Lawrence Erlbaum Associates, Inc., Publishers.

Slattery, P. (2008) *Curriculum development in the postmodern era*. London: Routledge.

White, J. (2005) *The Curriculum and the child: The selected works of John White*. Milton Park, Abingdon, Oxon (UK): Routledge.